**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) HALMASHAURI YA MANISPAA YA BUKOBA.**
***Shule ya Sekondari Kagemu, S.L.P 1232, Bukoba***

**Namba za simu:**
**Mkuu wa Shule: 0764890747/0621001943**
**Makamu Mkuu wa Shule: 0786720777/0752767188**
**Matron: 0752193114**
**Barua pepe: kagemusekondari@gmail.com** **Tarehe ……………**

Mzazi/Mlezi wa…………………………………
S.L.P ………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KAGEMU HALMASHAURI YA MANISPAA YA BUKOBA MKOA WA KAGERA MWAKA …………….**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika Shule hii mwaka ………………. Katika shule hii kuna tahasusi za **HKL,CBG na HGL.**

Shule ya Sekondari Kagemu ipo umbali wa Kilometa **5** Magharibi mwa Mji wa Bukoba. Nauli ya kutoka mjini hadi kufika shuleni si zaidi ya **Tsh. 2000/**- kwa pikipiki au **Tsh. 10,000/**- kwa bajaji/ TAX

Muhula wa Masomo utaanza tarehe **……………..,** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……………**.** Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………….**.**

**2: Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Kila mwanafunzi aripoti shuleni akiwa na bima ya afya/au Tsh. 50,400/-.**

**2.2 Sare za Shule**

i. Shati nyeupe **2** zenye mikono mirefu na zisizo na urembo wowote
ii. Soksi nyeupe Jozi **2** na viatu vyeusi vya kufunga na Kamba vyenye visigino vifupi vyenye kufunika miguu na Visivyo na urembo wowote.
iii. Nguo za michezo ambazo ni "**tracksuit**" ya Blue Bahari kitamba kizito
iv. Raba jozi moja
v . Sweta rangi ya kijani **(dark green)** yenye shingo ya round.
vi) Tai iwe rangi ya sketi damu ya mzee isiyo na michirizi yoyote
vii) Sketi Damu ya mzee **(2)** kitambaa Kizito yenye mshono wa

malinda box **8** mbele na **8** nyuma.

a) kwa waislamu washone sketi ndefu na Hijabu inayofunika kifua (Angalia picha iliyoambatanishwa)

viii) Nguo za nje ya darasa (shamba dress) sketi mbili (**2**) za kijivu (malinda box **8** mbele na **8** nyurna kitambaa cha Festeem nzito.

ix) T-shirt mbili (2) rangi nyekundu Nzito zenye kola – Zinapatikana shuleni kwa anayehitaji kununua shuleni kwa gharama ya **Tsh 16,000/@** yenye muhuri wa shule.

**2.3 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni**

i)Madaftari makubwa yasiyopungua **10 (counter books) 3Q** iii) Mkebe wa Hisabati (Mathematical set),Rula, kalamu za Wino na pencil za kutosha
muhula
v)Dictionary**(ADVANCED LEVEL KWA (HKL HGL)/** kamusi (**HKL**) vi)Karatasi (photocopy papers•**A4 DOUBLE A)** Ream **01** kwa muhula mbili (**02**) kwa
mwaka. Pamoja na Rude paper kwa ajili ya mazoezi.
vii) Scientific calculator **01** wanafunzi wa sayansi viii)
Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia ix)Mwavuli
wa mvua moja (1)
x)Mto moja (1) na foronya mbili (2) za rangi ya pinki xi) Mashuka
manne (4) ya pinki yasiyo na maua na blanketi moja (1) xii) Godoro
moja (1) la futi 3 na chandarua kimoja (l) cha mraba xiii) Jozi mbili
(2) ya kanga/vitenge
xiv) Sahani l, bakuli 1, kikombe l, kijiko l, vyombo vyote viwe vya bati/mfupa
xv)Toilet papers (karatasi za chooni) kumi(l0),pamoja na sabuni ya maji ltr 5
xvi) Kifaa cha maji ya kunywa (kidumu kidogo lita 3 au 5) xvii) Taulo (l)
xviii) Nguo za ndani (gaguro 2, chupi zisizopungua 6 na sidiria 3) xix)
Vifaa maalum vya matumizi ya msichana **(Always paketi 4)**
xx)Sabuni, mswaki, dawa ya meno, mafuta ya kujipaka, dawa ya Viatu
xxi) Fyekeo l, brush ngumu (ndefu,/fupi) ya kusugulia vyoo l **(CBG)**

xxii) Jembe moja lenye mpini **(HKL)** xxiii) Mfagio mmoja wa ndani na panga moja **(HGL)** xxiv) Ndoo ya kuchotea maji yenye ujazo wa lita 20 na beseni moja la kuogea kwa wote.

xxv) Fedha kidogo za maturnizi binafsi maana shule hutoa chakula.

xxvi) Nightdress l na Box file moja.

**2.3 Michango mbalimbali.**

Mwanafunzi atalipa **Tsh 80,000/=** kama mchango wa uendeshaji wa shule kwa mwaka
Fedha zote zilipwe kwenye akaunti ya shule kupitia A/C. **NMB 31801100125** Jina la akaunti ni **Kagemu Secondary School.** Mwanafunzi awasilishe nakala malipo iliyoandikwa Jina la Mwanafunzi wakati wa kuripoti.

**3: Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu **Na. 25** ya mwaka **1978** na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. **10** ya mwaka **1995**. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo

ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule. iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku ( Morning and evening Preparations). iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule. vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa. viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kutunza mali za shule.
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari au muuguzi wa shule
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**3.2 a/ Mwanafunzi awapo shuleni/ hapaswi kufanya yafuatayo**

i. Kufuga kucha ndefu ii. Kupaka rangi kwenye kucha, mdomo, kope au nyusi iii.Kutumia vipodozi
iv. Kukata au kusuka nywele kwa mitindo iliyotofauti na maelekezo ya shule.
v.Kuvaa nguo fupi au zinazobana mwili vi.Kushiriki matendo ya uhalifu na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi. vii.Kumiliki kifaa chochote kinachotumia umeme kama pasi, heater, tedio, simu
viii.Mwanafunzi awapo shuleni haruhusiwi kwenda nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

**b/ Heshima**

i. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kuamkia walimu, wafanyakazi wasio walimu pia mtu au mgeni yoyote anayemzidi umri anapopita na anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
ii. Mwanafunzi kama raia mwema, lazima aheshimu Bendera ya nchi ya na wimbo wa Taifa
iii. Matusi, lugha chafu na kupigana ni dalili yakukosa heshima

**c/ Utii**

i. Kila mwanafunzi hanabudi atii na kufuata maelekezo na maagizo ya viranja, walimu na wafanyakazi wasio walim u na watu W0te
ii. Mwanafunzi anapoitwa Mahali lazima aitike na kukimbia kuelekea kule aliko kiongozi anayemuita ikiwa ni mahali salama.
iii. Kiburi, majibu ya jeuri na matumizi ya lugha mbaya haviruhusiwi
iv. Ni wajibu kila mwanafunzi kufanya na kukamilisha kazi anayopangiwa iwe nje au ndani ya darasa

**d/ Upendo**

Mwanafunzi ajipende yeye mwenyewe na awapende wenzake kama ndugu zake wa shuleni awapende walimu kama wazazi Wake, aipende shule yake kama nyumbani kwake, aipende na kujivunia nchi yake ya Tanzania

**e/ Ruhusa**

Ruhusa maalumu ya kutoka nje ya shule itatolewa mara moja kwa muhula (shopping day) kutegemea na uongozi utakavyoamua.

**f/ Mambo ya msiba**

Mwanafunzi akifiwa akiwa shuleni taarifa zote zipitie kwenye ofisi ya Mkuu wa shule ruhusa ya Kwenda nyumbani itatolewa na Mkuu wa shule baada ya kuzingatia taratibu muhimu.

**Mabadiliko ya anwani**

Mzazi unashauriwa kutoa taarifa kwa Mkuu wa shule iwapo anwani inayotumika kwa mawasiliano imebadilika.

**h/ Ripoti**

Shule hutoa taarifa za maendeleo ya mwanafunzi kitabia, kitaaluma zitatumwa kila muhula.

**MUHIMU**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.3 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kufuga ndevu.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
viii. Uvutaji wa sigara.
ix. ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa.
x. Kupata mimba.
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi kinyume cha taratibu za mazingira ya shule.
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.



**4.Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya **(Medical Examination Form)** ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai; iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

Iii. Bandika picha za wazazi/walezi kama inavyoelekezwa kwenye **KIAMBATISHO B** ukurasa wa 8,

Aidha picha (passport size) ya mwanafunzi ibandikwe upande wa juu kulia kwenye fomu hiyo (**KIAMBATISHO B)** ukurasa wa 8.

**NB: Hakikisha viambatanisho vyote vinavyotakiwa kujazwa vimejazwa kwa usahihi na kukabidhiwa shuleni wakati wa kuripoti**.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**......................**

**SHUKURU D. SHEMBE**

**MKUU WA SHULE.**

**ANGALIZO: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa Shule: 0764890747**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0786720777/0752767188**
- **Mwandamizi Taaluma: 0744913650**
- **Matroni 0752-193114**

## AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi…………………………………………………………………………..mzazi/mlezi wa ………………………………………………...nimezisoma sharia za shule nikiwa na mwanangu na kujadili pamoja naye na amezielewa. Ninakubaliana kushirikiana na uongozi wa Shule katika malezi ya mwanangu na nitakubaliana na adhabu yoyote itakayoamuliwa na uongozi wa shule pale mwanangu atakapokiuka mojawapo ya sheria na kanuni hizi.

Saini ya mzazi/mlezi…………………………………tarehe…………………………………

## AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi ………………………………………………..wa kidato cha ……….. nimesoma kwa makini sheria na taratibu za Shule nikiwa na mzazi/mlezi wangu. Nimejadiliana naye na nimeelezwa vizuri kabisa. Ninaahidi kuwa nitazifuata na endapo nitakiuka mojawapo ya sheria na taratibu hizi hatua zichukuliwe dhidi yangu. Ewe mwenyezi Mungu nisaidie.

Saini ya mwanafunzi…………………………….Tarehe ……………………………

Ni imani yangu kuwa utafuata hizi sheria ili uweze kujifunza kwa bidii na kwa mafanikio yaliyo bora. Nakutakia kila la heri na karibu sana Kagemu Sekondari.

…………………

SHUKURU D.SHEMBE

**MKUU WA SHULE**

## KIAMBATISHO B

***Shule ya Sekondari Kagemu S. L. P 1232, Bukoba. Simu:*** **0764890747**
**Barua pepe: kagemusekondari@gmail.com**

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina la Mwanafunzi……………………………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………………………………
3. Mahali alipozaliwa: Mkoa ………………………
   Wilaya……………………………….
   Tarafa……………………………Kata …………………Kijiji/Mtaa…………...............
4. Dini…………………………………. Dhehebu…………………………………………….
5. Jina la baba mzazi/mlezi…………………………………………………
   Anuani……………………….. Namba ya simu……………………..
   Kazi ya baba mzazi/mlezi……………………………………………….
   Yuko hai? Ndiyo/ Hapana (kata isiyohusika)

6. Jina la mama mzazi/mlezi…………………………………………………..Anuani
   …………………… Namba ya simu………………………………………kazi ya mama mzazi/mlezi………………………………
   Yuko hai? Ndiyo/Hapana (kata isiyohusika)

7.Taja majina na anuani za walezi/Ndugu wengine wawili wasiokuwa wazazi wanaoruhusi wa kufika shuleni kuyasikiliza na kutoa maarnuzi juu ya mashauri ya młoto wako.

JINA................................................ANUANI...............................SIMUNA...................................

JINA.________________________ . ANUANI.................................. SIMUNA-..............…………....

8.Taja malina yawatuwatakao ruhusiwa kumtembelea młoto wako akiwa hapa shuleni

1……………………………………….Uhusiano ………………umri……..simu…………………….

2……………………………………….Uhusiano ………………umri……..simu…………………….

3……………………………………….Uhusiano ………………umri……..simu…………………….

A.Picha za wazazi

| | |
|---|---|
| | |

C.Picha za walezi

| | |
|---|---|
| | |

D. Picha za ndugu wengine kama wapo (sio łazima kama wanne wanatosha)

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |

*KIAMBATISHO C*

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**NAMEO F STUDENT…………………………………………………………………….**

To medical officer **I/C** of

………………………………………..District/ Regional/Referral/Designated Hospital,

**P.O BOX**…………………………..

Please examine the above named in full as to his physical and mental fitness for being able to pursue two years of Secondary School Education. In case of an acute Defect/disability in each category or subcategory may render the applicant ineligible of admission or eligible of admission to schools of students with special needs:-

**i.** Blood pressure……………………………………………………………….

**ii.** Sickle cell test…………………………………… iii. (a) Eyesight…………………………………… …

(b) Spleen………………………………………………

(c) Hearing………………………………………………………………

(d) Veneral diseases…………………………………………………………..

(e) Lepsory……………………………………………………………………….

(f) Typhoid………………………………………………………………………

iv.Neuroses………………………………………………

**v**. Other serious disease…………………………………………………………

General comment(s)……………………………………………………

Name………………………………………………………………………….

Designation……………………………………………………………

Official stamp…………………………… Date……………………………………

**ANGALIZO**: mzazi athibitishe kuwa vipimo hivi vimefanyika kikamilifu na siyo kujaza jina na saini ya Mganga. Atakayegundulika kuwa hakuchukua vipimo kihalali atarudishwa nyumabani.

KIAMBATISHO D

*Shule ya Sekondari Kagemu*
*S. L. P 6, Bukoba. Simu:* **0766877124**
Barua pepe: **kagemusekondaro@gmail.com**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI**

Mimi……………………………………………nakubali nafasi ya kidato cha tano niliyopewa na Shule ya Sekondari Nyakato. Ninaahidi kutii na kufuata kwa uaminifu sharia, kanuni na taratibu zote za shule, kujifunza kwa bidii, juhudi na maarifa kwa uwezo wangu wote ili kutimiza lengo la kufaulu kwa kiwango cha juu kwa faida yangu, familia yangu na Taifa kwa ujumla. **Ninaahidi kuripoti shuleni nikiwa nimevaa yunifomu kamili kama ilivyoelekezwa na kwa siku iliyopangwa bila kuchelewa**.

Saini ya mwanafunzi……………………

Tarehe ……………………………………

**MICHORO NA RICHA**








urefu wa sketi kutoka kwenye goti uwe cm l 5 kwenda chini upana wa pindo la sketi uwe cm 6 NB Mwanafunzi rnwenye matatizoya kifua ashone pull neck nyeupe au nyeusi.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.